JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 15- 2021/2022**

**DHIDI YA**

**RICHARD SHUKIA T/A ZAMAMPYA TV**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI MTANDAONI), 2020**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Tarehe 12/08/2022, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni kwa **Richard Shukia T/A ZamaMpya TV** kwa ajili ya kutoa huduma za utangazaji wa maudhui mtandaoni.

1.2 Mnamo tarehe 28/08/2022, Kituo cha televisheni cha **ZamaMpya** kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, kilichapisha taarifa za uchochezi ambazo zilikusudia kupotosha Umma, zinazodaiwa kutamkwa na Msanii wa Muziki ajulikanaye kwa jina la Selemani Msindi, maarufu kama Afande Sele.

1.3 Taarifa hiyo iliyoambatishwa na picha ya Msanii Afande Sele ilidai kuwa viongozi wamekosa ubunifu na kwamba ni maneno tu na hawaoni miradi ikiisha na kudai kuwa haya ni matokeo ya kuambiwa wale kwa urefu wa kamba zao. Taarifa hiyo ilisomeka kama ifuatavyo:

*"Tozo zimekuwa nyingi lakini watu hawaoni zinafanya kazi gani, hawaoni miradi ikiisha, ni maneno tu, mfano SGR/bwawa la umeme, watu wanachukizwa na tozo kwa sababu viongozi wamekosa ubunifu na lle kauli ya kuambiwa wale kadri ya urefu wa Kamba zao ndio matokeo yake haya".*




1.4 Uchapishaji huo uliofanywa na Kituo cha **ZamaMpya TV** unakiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji.

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Uchapishaji huo umekiuka Kanuni zifuatazo:

Kanuni za 9(a),12(a)(i) na 16(1) pamoja na Aya ya 3 (a), (d), (g), (h) na (k) ya Jedwali la Tatu katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni), 2020 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Marekebisho ya Kanuni za Maudhui Mtandaoni za Mwaka 2022, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*9. A licensee shall comply with all the terms and conditions of the licence and observe the following:*

*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

12. An Online Content Services License Category A shall be required to comply with the following conditions-

(a) in the case of online content service licensee, shall-

(i) adhere to journalism ethics and professional requirements as per the Media Services Act;

*16.-(1) A person shall not publish any prohibited content as set out in the Third Schedule*

***3. Public Security, Violence and National Safety***

*(a) content against the State and public order including content that aims to or publishes information, news, statements or rumors for the purpose of ridicule, abuse or harming the reputation, prestige or status of the United Republic, the flag of the United Republic, the national anthem or the United Republic's symbol, national anthem or its logos;*

*(d) content that would threaten the security of the United Republic or affect public order;*

*(g) content that incites, encourages or enables the commission of a crime against the United Republic or its citizens;*

*(h) content that is likely to threaten the stability of the United Republic or its safety, unity or security, or harming national unity or social peace;*

*(k) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime or leads to public disorder or that may threaten national security or public health and safety;*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

3.1 Tarehe 29/08/2022, Kamati ya Maudhui ilikiandikia Kituo cha **ZamaMpya TV,** wito wa kuwasilisha utetezi wa maandishi na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui tarehe 02/09/2022, Saa 05:00 Asubuhi ili kujieleza kwa nini hatua za kisheria

zisichukuliwe dhidi yake kwa kukiuka Kanuni za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni, 2020 kama zilivyoainishwa hapo juu.

3.2 Tarehe 02/09/2022, saa 05:00 Asubuhi, ZamaMpya walifika mbele ya Kamati kuwasilisha utetezi wao. Aidha ZamaMpya TV waliwakilishwa na Mawakili Paul Emmanuel Kilasa Kisabo na Onesmo Paul pamoja na Mabel Robert Nasua (intern), Flora Lyimo, Afisa Masoko na Richard Mrusha, Mpigapicha. Pia, iliwasilisha utetezi wake wa maandishi, uliosainiwa na Paul Emmanuel Kilasa Kisabo.

3.3 Licha ya wawakilishi tajwa hapo juu waliofika mbele ya Kamati siku ya usikilizwaji wa shauri, Kamati ilibaini umuhimu/hitaji la uongozi wa juu wa ZamaMpya TV kufika mbele ya Kamati kutokana na shauri husika kujumuisha maswala ya kisheria pamoja na weledi katika fani ya Utangazaji wa Habari. Hivyo Kamati iliahirisha usikilizwaji wa shauri mpaka tarehe 05/09/2022, Saa 05:00 Asubuhi ili kuupatia nafasi Uongozi wa juu wa Zamampya TV uweze kufika mbele ya Kamati siku ya usikilizwaji wa Shauri hilo.

3.4 Tarehe 05/09/2022, Saa 05:00 Asubuhi, **ZamaMpya TV** ilifika mbele na Kamati kutoa utetezi wake ikiwakilishwa na Mawakili Paul Emmanuel Kilasa Kisabo na Rehema Mwakyusa, Mayasa Khatibu, (Intern) na Abdallah Khamis, Mhariri wa Kituo.

## 4.0 KUSOMEWA MASHTAKA NA KUANGALIA MAUDHUI YA ZAMAMPYA TV YANAYOTUHUMIWA.

Kamati ya Maudhui ilikisomea Kituo cha **ZAMAMPYA TV** mashtaka yake. Pia, Kamati na wawakilishi wa Kituo hicho kwa pamoja waliangalia maudhui yaliyochapishwa tarehe 28/8/2022 kwenye ukurasa rasmi wa twitter wa kituo hicho na uongozi wa ZamaMpya TV walikiri kuwa chapisho hilo ni la kwao. Hivyo Kamati iliualika uongozi wa ZamaMpya kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

## 5.0 UTETEZI WA ZAMAMPYA TV

**ZamaMpya TV** waliwasilisha hoja za utetezi wao kwa njia ya maandishi na kwa mdomo kama ifuatavyo:

5.1 **ZamaMpya TV** walianza kwa kupinga tuhuma dhidi yao na kudai kuwa taarifa waliyoichapisha haikuwa na uchochezi wala yenye kukusudia kupotosha umma. Walidai kuwa Kituo chao hakina madhumuni/malengo ya kuchapisha maudhui ya kuchochea wala kupotosha umma na badala yake wanafanya kazi yao ya Uandishi na Utangazaji wa Habari kwa kutafuta taarifa na kisha kuzitoa/kuzichapisha kulingana na Sheria za nchi, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa Ibara ya 18, Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016 pamoja na Sheria zinazoongoza vyombo vya Habari mtandaoni kama Kanuni ya Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni;

5.2 **ZamaMpya TV** waliendelea kujitetea kuwa wanaposoma taarifa yao waliyoichapisha, wanashindwa kujikita kwenye maelezo na kufanya utetezi sahihi kwa maana hawajui ni kipi cha uchochezi au kinachokusudia kupotosha umma katika taarifa waliyochapisha, kwamba wito haujawa wazi wala haujaeleza kinagaubaga kwamba ni nani alichochewa na ni madhara gani yalitokea/kufanyika baada ya kuchochewa;

5.3 **ZamaMpya TV** pia walijitetea kwa hoja kwamba chanzo cha taarifa waliyoichapisha ni Msanii wa Muziki, Selemani Msindi, maarufu kama Afande Sele ambaye hayupo kwenye mashtaka kama muhusika muhimu wakati yeye ndiye aliyetamka maneno yaliyochapishwa na hivyo yeye ndio angeweza kufafanua au kueleza maana ya maneno aliyoyatamka kama alikusudia kufanya uchochezi na kupotosha umma. Walidai wanaamini kuwa kuchapisha taarifa kinyume na mtoaji alivyosema ndio kupotosha umma lakini kuchapisha taarifa kama ilivyotolewa na mtoa taarifa kama walivyofanya **ZamaMpya TV** sio kupotosha umma wala uchochezi. Kwamba Kituo chao kina haki na wajibu wa kutafuta na kutoa taarifa kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na hivyo hakuna ukiukwaji uliofanyika;

5.4 **ZamaMpya TV** waliendelea kudai kuwa chombo cha kutoa taarifa kinapaswa kuchapisha taarifa za kweli na ambazo kimezitafuta chenyewe na waliomba kuichambua taarifa yao ili kuiridhisha Kamati kuwa haikuwa ya uchochezi wala upotoshaji kwa umma. Walisema maswali ya kujiuliza kuhusu taarifa ya tozo waliyochapisha ni je, tozo ni zipi? Je, ni kweli tozo hazijawa nyingi? Na zinafanya kazi gani? Je, miradi gani imeisha kwa tozo? Je, ni kweli watu hawachukizwi na

tozo? na kwamba maswali haya yote yanaweza kujibiwa na mtoa taarifa mwenyewe na sio **ZamaMpya TV**;

5.5 Walieleza kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Serikali hupata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Kwamba lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi. Kwamba, Ibara tajwa inatoa msingi/haki wa wananchi kuhoji Serikali yao juu ya ustawi wao, kupitia njia mbalimbali zikiwemo kupitia chombo cha habari au mahakamani na kutoa maoni yao kuhusu jinsi wanavyoziona tozo na mambo mengine yahusuyo wao na Serikali yao. Kwa mfano, kama kuna tozo nyingi, wananchi wana haki ya kuhoji kama zinapelekea ustawi wao au hapana. Kwamba, ili Serikali itekeleze lengo lake la ustawi wa wananchi, ni lazima viongozi wawe wabunifu kwenye vitu vyenye tija/manufaa kwa wananchi na tofauti na hivyo, wananchi wanaweza kuhoji kama ubunifu una tija au vinginevyo. Waliongeza kuwa Ibara tajwa ndiyo msingi wa chombo cha habari kutafuta habari kutoka kwa mtoaji na kisha kuzichapisha kwa sababu inampa kila mtu haki ya kutoa maoni na kueleza fikra zake;

5.6 Kuhusu kauli waliyochapisha ya kwamba "...na ile kauli ya kuambiwa wale kadri ya urefu wa kamba zao ndio matokeo yake haya", **ZamaMpya TV** walijitetea kuwa kuna maswali ya kujiuliza ambayo ni Je, kauli hii ilishawahi kutolewa? Je, ina maana gani? Je, imepelekea matokeo gani? Na kwamba maswali haya pia yanaweza kujibiwa vizuri na mtoa taarifa lakini sio wao waliyochapisha taarifa hiyo;

5.7 Aidha, **ZamaMpya TV** walijitetea kuwa kosa la uchochezi (yaani "Sedition" kwa lugha ya Kingereza) wanalotuhumiwa nalo halitajwi katika Kanuni yoyote kati ya Kanuni za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni wanazotuhumiwa nazo. Walidai kuwa Kanuni ya 9 (a) haihusiani na uchochezi bali inamtaka mtoa huduma kuhakikisha kuwa maudhui mtandaoni ni salama na hayakiuki Sheria yoyote. Kwamba, Kanuni ya 12 (a) (i) inasisitiza uzingatiaji wa Misingi na Maadili ya taaluma ya Habari ambavyo hawajavikiuka. Kwamba, maudhui yao waliyochapisha hayakiuki Kanuni ya 16 (a) na Aya ya 3 (a), (d), (g), (h) na (k) kwa sababu hayakiuki Amri za Serikali, hayahatarishi ulinzi,usalama na umoja wa nchi na wala hayachochei kutendeka kwa makosa;

5.8 Waliendelea kueleza kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 20 ya Kanuni za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni, endapo mtoa huduma wa maudhui mtandaoni atachapisha maudhui yoyote yaliyokatazwa, basi mlalamikaji atatakiwa kuwasilisha lalamiko lake kwa mtoa huduma husika ili lipatiwe suluhisho ndani na masaa kumi na mbili (12) na endapo mtoa huduma atashindwa, mlalamikaji atawasilisha lalamiko lake kwa mamlaka ndani ya siku thelathini (30). Walidai kuwa katika shauri hili, utaratibu huu haukuzingatiwa kwa sababu hakuna lalamiko lolote lililowahi kuwasilishwa kwa **ZamaMpya TV**.

5.9 Aidha, walieleza kuwa Ibara ya 19 ya "*Universal Declaration of Human Rights*", ambayo Tanzania imesaini, inatoa uhuru wa mtu kueleza fikra na maoni yake.

5.10 Wakati walipoulizwa maswali ya ufafanuzi na Kamati, walisema kuwa kwa sasa nchi yetu ina ajenda ya tozo ambapo wapo wenye mawazo chanya na hasi pia. Kwamba jukumu lao kama waandishi wa habari ni kutoegemea upande wowote na wamelitekeleza jukumu hilo na ndio maana tayari Serikali imeshaanza kushughulikia suala hili. Kwamba, wanaomba wasifungwe mikono katika kutekeleza wajibu wao wa kisheria na kimaadili katika kuuhabarisha umma. Walidai kuwa kwa kuwa uandishi wa mtandao wa "twitter" hauna uwezo wa kubeba habari yote katika chapisho moja, walishawahi pia kuchapisha maoni ya watu wengine waliosifia na kuelezea umuhimu wa tozo, ambao ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mchungaji Antony Lusekelo, tarehe 03/09/2022 na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, Mb, tarehe 01/09/2022.

5.11 Hata hivyo, wakati wakiendelea kuulizwa maswali ya ufafanuzi na Kamati, **ZamaMpya TV**, walijibu kuwa maudhui yanayotuhumiwa walishayaondoa katika mtandao wao kwa sababu mara baada ya kupokea wito wa mashtaka wa Kamati, waliona kwa kuwa maudhui yanadaiwa kuwa na hisia za uchochezi na upotoshaji, ni busara wayaondoe kabla ya kuja kusikilizwa na Kamati.

5.12 Kwa mujibu wa utetezi wao hapo juu, **ZamaMpya TV** iliiomba Kamati iifutie mashtaka yao kwa maana hakuna ukiukwaji uliofanyika.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imezingatia utetezi wote uliowasilishwa na **ZamaMpya TV**. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa **Zamampya TV** imetenda kosa la kuchapisha taarifa/maudhui yaliyokusudia kuupotosha umma na pia kuuchochea ("incite" kwa lugha ya Kingereza) umma kwa kitendo chao cha kuchapisha maudhui hasi yaliyohusu tozo na yaliyoegemea upande mmoja kwa kuwashutumu na kuwatuhumu Viongozi bila kuwapa nafasi ya kujibu katika taarifa hiyo. Taarifa hiyo haikuwa na mizania,ulinganifu na usahihi. **ZamaMpya TV**, kama chombo cha habari kilipaswa kuzingatia Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari kwa kufanya uchambuzi/utafiti sahihi wa taarifa waliyoipata kutoka katika chanzo chao, ikiwa ni pamoja na kuwahoji wahusika wa upande uliotuhumiwa na taarifa yao (serikali) kabla ya kuchapisha ili kutoa taarifa sahihi na kamili. Kamati imebaini kuwa taarifa iliyochapishwa na **ZamaMpya TV** sio salama, haikuzingatia maadili na inauchochea umma kutenda vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani,utulivu, usalama na umoja wa nchi. Hivyo basi, maudhui hayo yanakiuka Kanuni za 9(a),12(a)(i) na 16(1) pamoja na Aya ya 3 (a), (d), (g), (h) na (k) ya Jedwali la Tatu katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni), 2020;

6.2 Kamati imeona kuwa hoja ya **ZamaMpya TV** kuwa uendeshaji wa shauri hili haukuzingatia matakwa ya Kanuni ya 20 ya Kanuni za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni, 2020 haina msingi wowote kisheria kwa sababu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kama msimamizi/mdhibiti ("Regulator") wa sekta ya mawasiliano nchini Tanzania ina wajibu wa kulinda maslahi ya Serikali, watoa huduma za mawasiliano na watumiaji/walaji wa huduma za mawasiliano pia. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura 172, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina mamlaka ya kufuatilia na kuchukua hatua dhidi ya mtoa huduma za maudhui aliyekiuka Sheria, Kanuni na Maadili hata kama hakuna mlalamikaji aliyelalamika kwa kufuata utaratibu wa Kanuni tajwa ya 20;

6.3 Pia, Kamati imeona kuwa hoja ya **ZamaMpya TV** kuwa walishawahi kuchapisha taarifa nyingine za watu waliosifia tozo haina mashiko kwa sababu Kamati imebaini kuwa taarifa hizo nyingine zilichapishwa katika siku nne hadi sita baada ya taarifa hasi kuchapishwa. Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari yanawataka watoa huduma kutafuta uchambuzi/ufafanuzi wa kina na kutoa taarifa

kamili isiyo na dosari wala kuegemea upande mmoja katika chapisho hilo hilo moja;

6.4 Aidha, Kamati imebaini kuwa hoja za **ZamaMpya TV** kuwa ufafanuzi wa taarifa waliyoichapisha unatakiwa kufanywa na Afande Sele mwenyewe (chanzo cha taarifa) na kwamba Katiba ya nchi na "Universal Declaration of Human Rights" zinampa mtu yeyote haki ya kuhoji na kueleza maoni/fikra zake hazina mashiko kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni ya 9 (a) ya Kanuni tajwa za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni, **ZamaMpya TV** ambaye ndiye amepewa dhamana/leseni ya kutoa maudhui anapaswa kisheria kuhakikisha anachapisha maudhui sahihi na yaliyofanyiwa uchambuzi wa kina wa kubaini ukweli wake baada ya kuyapokea kutoka katika vyanzo vyake na kabla ya kuyapeleka hewani. Pia, chombo cha habari kina wajibu wa kisheria wa kuhakikisha kuwa maoni, hoja au fikra zozote zinazotolewa kupitia chombo husika zinazingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

6.5 Kamati imebaini kuwa hoja ya **ZamaMpya TV** kuwa katika maudhui waliyochapisha kuna maswali kadhaa ya kujiuliza ambayo yalitakiwa kujibiwa/kufafanuliwa na Afande Sele mwenyewe haina mashiko yoyote kwa sababu wao kama chombo cha habari ndiyo walitakiwa kufanya uchambuzi wa maswali hayo yote na kuyatafutia ufafanuzi kutoka kwa sehemu zote zinazohusika ili kuchapisha taarifa kamili na isiyo na dosari;

6.6 Kamati imebaini kuwa kitendo cha **ZamaMpya TV** kukiri kuyaondoa maudhui yao yanayotuhumiwa mtandaoni kabla ya kufika mbele ya Kamati kwa sababu kuwa yalikuwa yamepata hisia za uchochezi na upotoshaji, kinaonesha wazi kuwa tayari walishagundua dosari na ukiukaji wa Kanuni katika maudhui yao hayo.

6.7 Mwisho, Kamati imejiridhisha kuwa **ZamaMpya TV** imekosa umakini katika usimamizi, utayarishaji na uchapishaji wa maudhui yao mtandaoni, hivyo kupelekea ukiukwaji wa Kanuni tajwa.

## 7.0 MAELEKEZO YA KAMATI KWA ZAMAMPYA TV

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaielekeza **ZamaMpya TV**:

7.1 Kuhakikisha inazingatia Misingi, Sheria, Kanuni, Maadili, Weledi, Vigezo na Viwango vya tasnia ya Uandishi na Utangazaji wa Habari katika

kutayarisha/kuandaa, kusimamia/kuhariri, kufuatilia, kutathmini, kuchambua, kuweka mizania na kutangaza maudhui yao mtandaoni;

7.2 Aidha, kituo cha ZamaMpya TV kinatakiwa kuwajibika kwa kila maudhui yanayochapishwa katika mitandao yake ili kukidhi matakwa ya Sheria, Kanuni pamoja na maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

**8.0 UAMUZI WA KAMATI**

8.1 Baada ya kupokea na kutafakari kwa kina utetezi wa **ZamaMpya TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **ZamaMpya TV** imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni), 2020 kama ilivyofanyiwa Marekebisho Mwaka 2022 na ilivyoainishwa katika Tathmini ya Kamati hapo juu.

8.2 Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (3) (a) na (d) ya Kanuni tajwa za Utangazaji wa Maudhui Mtandaoni, 2020, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **ZamaMpya TV:**

1. Inapewa Onyo;

2. Inaamuriwa kulipa faini ya Shilingi za Kitanzania Milioni Mbili (TZS. 2,000,000/=) tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ndani ya siku ishirini na moja (21) tokea kusomwa kwa uamuzi huu;

3. Inawekwa chini ya Uangalizi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kipindi cha muda wa miezi mitatu (3). Katika kipindi hicho cha miezi mitatu, ZamaMpya TV inatakiwa kuboresha utendaji kazi wake na mfumo wake wa usimamizi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya taaluma ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **09 Septemba, 2022**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Ndalahwa Habbi Gunze**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..........................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Derek Kaitira Murusuri** ....................................

2. **Jacob Gregory Tesha** ....................................